**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

# WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

## TAARIFA KWA UMMA

### UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA KAMPUNI BAADA YA USAJILI

Dar es Salaam - 06 Januari, 2026.

Msajili wa Kampuni anapenda kuwataarifu Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa Kampuni kuhusu wajibu wa kisheria wa kuwasilisha kwa Msajili wa Makampuni Taarifa za Mwaka na Mizania (Annual Returns and Audited Accounts) za Kampuni kama Sheria ilivyoelekeza kwa mujibu wa Kifungu 131 cha Sheria ya Kampuni, Sura 212 toleo la mwaka 2023.

Sheria pia, inataka Kampuni za Kigeni (Foreign Companies) kuwasilisha Hesabu za Mwaka kila mwisho wa mwaka (Calendar Year). Taarifa hizi zinatakiwa kuwasilishwa kwa Msajili wa Kampuni kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (anniversary of incorporation) au tarehe nyingine yoyote ambayo Kampuni itakuwa imeichagua na kumtaarifu Msajili wa Kampuni nae akaridhia.

Aidha, kwa kampuni ambayo haijakidhi takwa hili haitaweza kufanya mabadiliko ya taarifa yoyote yanayoletwa na kampuni hayatafanyiwa kazi mpaka Kampuni husika itakapokuwa imewasilisha Taarifa zake za Mwaka.

Taarifa za Mwaka na Mahesabu ya Mwaka kwa kampuni za kigeni (Foreign Companies) husaidia kutoa taswira halisi ya Kampuni, hivyo humuwezesha Msajili wa Kampuni kuwa na taarifa sahihi za Kampuni husika. Kampuni zinahimizwa kuwasilisha Taarifa za Mwaka ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea wakati kampuni zinawasilisha taarifa za mabadiliko mbalimbali ya kiutendaji yaliyotokea katika kampuni hizo.

Kwa usaidizi wa karibu wasiliana nasi kwa simu namba +255(0) 222 212 800.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma**